

Sehemu za kitabu

Madondoo toka kitabu cha Gabriele,
nabii na mjumbe wa Mungu:

Haukutelekezwa! Mungu yu karibu nawe kwa maneno na kwa matendo

Vijitabu vitolewavyo bila malipo

- Kumpata Mungu! Wapi? Na Vipi?
- Maisha ya raha hadi uzeeni
- Usikate tamaa! Stahimili!
- Mungu ndani mwetu
- Hauko peke yako
- Mafundisho ya Yesu Mlimani
- Mnaishi milele. Hakuna mauti
- Yesu na wanyama
- Hili ni Neno Langu A na Ω
- Uwezekano wa kuzaliwa upya katika mwili wa mwanadamu ni neema ya Uzima



First Edition in Swahili: August 2023
1ère édition en Swahili: Août 2023

The German edition is the work of reference
for all questions regarding the meaning of the contents
Pour toute question se rapportant au sens,
l'édition allemande fait référence

© All Rights Reserved / Tous droits réservés
Gabriele-Verlag Das Wort GmbH

Maneno ya Baba wa mbinguni
kwa wanae Wanadamu
na pia maneno ya Kristo

Wanangu na binti Zangu! Ikiwa dhamiri yenu inajitoa kwangu kwa dhati, Mimi Roho wa ulimwenguni pote, basi vivuli vinavyoitia bado giza mioyo yenu na kuwatupa gizani mara na mara bila ulinzi vitatoweka.

Kusudi dhamiri yako ibaki daima karibu nami, unapaswa kukubali yote yaliyo. Ukubali una ukuu ndani mwake.

Mara tu unapokubali mateso yako, unaongeza nguvu chanya ambayo ni Mimi. Mimi, Uzima, nitaanza basi kutenda kazi ndani ya wasiwasi na shida zako, na nitakuletea maisha chanya, raha, afya na mafanikio.

Kukubali kikamilifu matukio yote, hatima ya mtu na kila kitu, huleta utulivu wa ndani.

Kubali vyote kwa shukrani.
Baadaye utajaa furaha na upendo.
Wasiwasi, shida na mateso yako vitatoweka ukivikubali kwa shukrani.

Shukrani ni chemchem ya nguvu. Shukrani ya kweli ni sawa na kuishi maisha chanya. Mtu anayehisi, anayefikiri na kusema vyema, anaishi kwa kweli; anatoa shukrani daima. Hivyo, nguvu chanya za ulimwengu zinamhudumia. Nguvu chanya zinamletea furaha, upendo, maelewano, matumaini na amani.

Anakuwa huru toka wasiwasi, shida, na mateso, kwani katika shukrani ya kweli hamna mateso na wasiwasi ya kidunia.

Shukrani ina ukuu ndani mwake.

Shukrani halisi ina ndani mwake matumaini kwa Mungu, uhakika kwamba Yeye, Sheria ya milele, huongoza yote yawe mema.

Ndani ya shukrani mna pia hisia ya usalama na ukaribu na Mungu, ambaye kwa upande wake analeta amani ya ndani.

Mtu anayejaa amani, anajaa pia upendo. Hana ubinafsi.

Roho wa Mungu basi hujidhihirisha kutoka kwenye kina cha nafsi yake. Kama waridi, mtu anayejazwa na Mungu hueneza manukato takatifu ya Yule aliye milele.

Shukrani ina ndani mwake matumaini, faraja na uaminifu.

Wanangu, tambueni kwamba ndani ya kila kitu mna nguvu chanya, hata kama, kwa mtazamo wa kwanza, kila kitu kinaonekana kuwa kibaya.

Uovu peke yake hauwezi kudumu.

Ndani ya mambo hasi mna nguvu chanya pia, kiini cha uzima kinachotenda kazi. Nguvu isiyoweza kuharibika, Mungu, anatamani kuwa hai ndani ya nafsi na ndani ya mwanadamu.

Mtu anayeishi ndani Mwangu atatambua kwa wakati shida zinazojitokeza na atazishinda pia kwa msaada wa nguvu toka Uzima Wangu. Mtu asiyetambua pa wakati shida, huzirudilia mara na mara katika fikra na katika maneno. Kwa namna hiyo, inawezekana magumu hiyo yageuke shida zilizobaki bila suluhisho miaka mingi.

Okiwa uko tayari kunikabidhi makosa na udhaifu wako, basi haya yanaweza kubadilishwa ndani mwako, kwa jumla au kwa sehemu.

Okiwa pia unanitambua Mimi katika ugonjwa, dhiki, wasiwasi na shida zako na unanikubali Mimi, sehemu chanya katika yote unayoyataja kuwa ni mambo hasi, basi nguvu hiyo chanya, yaani Mimi, Uzima wenye uwezo wote, Nitafuta uovu na nitageuza yote yaliyo hasi kuwa uzima chanya.

Nguvu Yangu chanya, Mimi Yule Aliye ,inatenda kazi katika kila hali, hata katika hali mbovu. Mtu anayeweza kuzungumza Nami, nuru asilia, hata katika hali mbovu atashinda na kutawala hali zote na matukio iliyopangwa ya maisha yake.

Nikabidhi mambo yote unayoyatambua, yanayokushinda, mawazo yote yanayokusumbua, na uwe huru ili sababu ambazo bado zipo ndani ya nafsi yako zipunguzwe au kufutika kabla hazijatoa matokeo yake.

Katika jambo lote mbaya mnapatikana pia nguvu chanya.

Yule anayejua kutambua hali hiyo chanya kwa wakati muafaka na kusimulia nayo atashinda hali mbovu ambayo inajitokeza wakati wote katika mazingira ya kimwili. Baadhi ya hali zingeweza kudhibitiwa ikiwa muda ule ule mlijikabidhi kwangu nafsini mwenu, mahali ambapo Ninaishi, Mimi, nuru ya kati.

Hebu acha kwa moyo wote nuru ya kiroho ing'ae! Heshimu na penda nguvu ya kiroho na baki tu ukiungana Nami daima, Mimi nguvu ya ulimwenguni pote, (...) ukijihisi daima ndani ya uzima wa Mungu.

Oshi ukiwa na msingi ndani mwako na utaishi maisha adilifu ulimwenguni humu. Kwa hiyo utastarehe ndani ya Mungu, uzima halisi, na Mungu, Uzima, hutenda kazi kupitia wewe.

Mnaweza kuwa karibu na wengine na kuwahudumia iwapo tu kidhamiri mpo karibu Nami, ninayemhudumia kila mtu.

Wale ambao kupitia hisia na mawazo yao wanafungamana na jirani zao, wamekwisha fungamana na mapenzi ya jirani zao.

Wale wanaoshikiliwa na mali na utajiri wanatawaliwa na nia ya kumiliki.

Wale wanaotegemea watu wengine, kwa kutegemea mawazo na matamanio yao, wanayoyakubali na kuyatekeleza maishani mwao, wanajifunga wenyewe kwa mapenzi ya watu hao na kwa hiyo wao si watu huru. Hawako huru kwa sababu wanafanya mapenzi ya watu wengine.

Uhusiano wa Mungu, Baba yetu, na wanae unajengwa juu ya msingi wa uamuzi huru.

Mtu aliyepata uhuru katika Mungu, anaishi kwa uangalifu kama mwana wa Mungu,

yuko huru na anaishi katika umoja na aina zote za viumbe.

Sheria Yangu, inafundisha kwamba wanangu hawapaswi kuishi katika upweke. Hata hivyo, iwapo unaishi katika upweke wa ndani na wa nje, jiswali ni hali gani inayokutawala bado na isiyovutia jirani yako kwako, ili uishi peke yako kwa muda.

Mwanangu, Jizoeze hekima: Dumisha uelewano na upole kwa jirani yako!

Umepewa nguvu ya kujitathmini wewe mwenyewe ili uendeleze hali hizo zote na kufikia upendo Wangu safi ambao ni utu wako halisi.

Kabiliana na manunguniko yako!

Pambana nayo. Kwa kuwa manunguniko inakuvuta kwenye bonde la huzuni na kukata tamaa.

Hebu, kila mmoja ajichunguze mwenyewe na atambue kiwango alichokifikia! Jitazame kwenye kioo, tazama tabasamu lako. Chunguza mwendo wa mwili wako. Sikiliza mlio murua wa maneno yako.

Chunguza kwa uangalifu mawazo yako. Mtu ambaye fikra zake bado zinazunguka tu kando ya utu wake binafsi ana ukungu wa utu wake duni. Hivyo, anaifunika nuru Yangu.

Ikiwa unataka kujitambua vema zaidi, sikiliza kwa makini maneno yako wewe mwenyewe, chunguza maneno unayoyasema na jinsi unavyoyasema. Maneno yako yanakutambulisha wewe ni nani.

Mwenyewe unaonyesha kwa watu walio karibu nawe ikiwa Roho, Uzima ambao ni Mimi, unang'aa kupitia wewe au kama utu wako duni bado inajidhihirisha.

Yule aliyepata amani ya ndani anaanza kumulika nuru ndani mwake kabisa. Na, kama nilivyofunua, mtu anayeng'aa hivyo hataishi katika upweke na kutengwa.

Ni watu wengi kabisa wanaotua matatizo na shida zao miguuni Pangu ila baadaye wanazichukua tena katika fikra. Kwa nini?

Kwa sababu hawaniamini na hatimaye wanataka kutumia ubinafsi wao kama turufu katika ulimwengu huu. Bado wanataka kutumia shida, magumu, na pia maradhi yao, kwa madhumuni fulani, iwe kwa kuzusha hisia ya huruma, au kuwalazimisha wenzao au kujitukuza.

Hali hiyo kama hali nyingine nyingi za utu wa mwanadamu huongeza tu magumu, matatizo na magonjwa, kwa sababu kila wazo linalotolewa katika mwelekeo huo ni nguvu ambayo inaendelea kudumisha shida na matatizo hayo.



Mtu anayeungana kiroho na jirani yake kupitia upendo hataishi kamwe katika upweke. Wale wanaoshiriki imani moja nawe watakushiriki na kuwa pamoja nawe. Watakuzunguka, wataishi nawe kwa upendo, na watabeba pamoja nawe mzigo ambao wewe mwenyewe ungepaswa kuubeba kulingana na sheria ya sababu na matokeo.

Mtakie jirani yako mambo mema, mambo yenye thamani zaidi na mazuri zaidi na hatua kwa hatua, utu wako utang'aa.

Elewa kwamba, kitu kinachowaunga watu wasio na ubinafsi wanaoshiriki maadili moja ni umoja katika roho Wangu,ni Sheria ya upendo inayowabeba na kuwasaidia.

Anayependa bila ubinafsi amezungukwa na watu wasio na ubinafsi, kwani vitu vinavyofanana hujikusanya pamoja. Utapewa kulingana na upendo wako na kulingana na kile unachokitoa.

Watu wa Kiroho hawana matarajio kwa wengine.

Anayeishi maisha ya kimwili na kupitia mwili anasubiri nuru itokee nje ili impe bidii na kumtia nguvu. Lakini faraja ya nje ni ya muda kitambo, haidumu.

Yule anayetegemea kile kinachotokea nje, kwa mfano maneno mazuri au tabasamu ya jirani yake, ana tabia ya matarajio. Hali hiyo ya matarajio daima husababisha tamaa zaidi. Mtu huyo anamtegemea sana jirani yake, ambaye daima anatarajia amfanyie mengi.

Mtu kama huyo anatarajia sana kuambiwa maneno mazuri, maneno ya kumsifu na maneno au matendo mengine kama na hayo. Hivyo ndivyo mtu maskini kiroho hujipa thamani mwenyewe kupitia watu wengine kama yeye.



Kitu ambacho mtu anataka kuhifadhi, atakipoteza. Kwa upande mwingine, mtu atahifadhi kitu alichoacha kwa manufaa ya wote na atapokea vingi vya ziada.

Mtu anaweza kuwa tajiri katika uzima huu, bali akawa maskini katika uzima ujao. Yote yanategemea jinsi anavyotumia utajiri wake wa kidunia. Akijiwekea mwenyewe utajiri huo, ataupoteza. Ila akiwa tayari kuutumia kwa manufaa ya wote, atabaki tajiri kiroho kama vile kimwili.

Uwe mwenye busara na mvumilivu!

Onyesha uelewa na huruma kwa jirani yako!

Hivyo utakuwa mtu asiye na ubinafsi na kamwe hutakuwa mpweke, mtu aliyetengwa.



Fahamu uwepo Wangu! Mimi ni nguvu.

Yule anayetaka kufikia dhamiri kuu, Mungu, lazima akuze hali zote nzuri ndani mwake, nafsini mwake. Haitoshi tu kwake kuzitambua, lazima aziishi, yaani, azitimize kila siku.

Upendo wangu usio na ubinafsi ndio nguvu iliyo ndani mwako. Nguvu ya Uzima ndiyo utu wako halisi. Fahamu chanzo chako, utu wako wa kweli!

Upendo bila ubinafsi ni uhusiano usioweza kuvunjika kati ya Baba na mwanae.

Upendo usio na ubinafsi ndio nguvu asilia ambamo ulitokea na ambapo utarudi kupitia Kristo, Mwanangu, Mkombozi wako.

Kidhamiri geukeni wana na binti wa Mungu! (...) Yule aliyenikubali Mimi na kunikaribisha ndani mwake na anayeishi katika Sheria ya msingi, anaishi kweli. Anaishi kwa uangalifu, anaishi uwepo wa kweli wa nafsi yake,yaani Mungu.

Mungu yupo, nawe ni nuru kutoka nuru yake na nguvu kutoka nguvu zake. Mimi ndimi nuru ndani mwenu na mngepaswa kubeba nami nuru ya Baba katika ulimwengu huu.

Ninaishi nawe. 0, nipe Mimi kila siku sana uwezekano wa kuishi kupitia wewe.

Chemchemi inaendelea kutiririka. Bado chemchemi iko kila mahali. Inakuchangamsha na kukulisha. Inakuburudisha na kukupa nguvu ili uweze kutoa nawe.



Jitahidi kuona mema katika mambo yote na ndipo uweze kuwahudumia wanadamu wenzako kwa kweli.

Nuru yangu inang'aa ndani mwako.

Inatamani kuangazia mbali kupitia wewe na kumulikia watu wengi wanaotaka kufuata njia ya amani na upendo, watu walio tayari kuleta nuru Yangu kwa watu wote na viumbe vyote ili iwe hivyo Duniani kama mbinguni.

Kila mtu mara na mara ana fursa ya kutafakari. Mabadiliko mabaya ya hali ya maisha au shida zingine ni maonyo yanayopaswa kututuma tutafakari.


Tumia vema wakati kwa manufaa yako!



Roho huru – Mungu ndani mwetu

Kitabu hiki kinamwelekeza msomaji kwenye njia ya uhuru na kinamuwezesha kujitenga na imani potovu, mila ngumu na taasisi zinazotushikilia. Njia hiyo ni njia iongozayo kwa Mungu, kwa Mungu ndani mwetu.

S179SW • ISBN 978-3-96446-247-3 • Kurasa 76



Yesu wa Nazareti alikuwa nani?

Utoto na ujana wake

Kitabuni humu mmekusanywa vifungu tofauti vya ufunuo wa Kristo, ambamo mwenyewe anaeleza hadithi ya maisha yake duniani katika Yesu wa Nazareti, kwa upekee ujana na utoto wake.

S170SW • ISBN 978-3-96446-226-8 • Kurasa 46



Jifunze kuomba

Katika sala ya kweli, unapata maarifa ya Mungu. Sala halisi humfanya mtu awe mwenye raha.

Ila, sala halisi inahitaji mafunzo. Kwa kuwa sala halisi tunayoifanya ndani mwetu wenyewe ni mazungumzo na Mungu.

S174SW • ISBN 978-3-96446-225-1 • Kurasa 54



Amri Kumi za Mungu zilizotolewa kupitia Musa

na kufafanuliwa katika usemi wa siku hizi, ni mashauri ya uzima yenye thamani kubwa inayomwezesha mtu kupata Amani ya roho, uhuru na kumsaidia kumkaribia hauta kwa hatua Mungu, Roho huru aliye ndani mwetu na ndani ya viumbe vyote.

S338SW • ISBN 978-3-96446-227-5 • Kurasa 46

Vitabu vingine vinapatikana katika lugha ya Kiswahili, kiingereza, kifaransa na nyingine nyingi tena

Infos at WhatsApp/Viber in English: +49 151 1883 8742
Infos par WhatsApp en français: +49 159 08 45 45 05
www.gabriele-publishing.com



Gabriele Publishing
The Word

Max-Braun-Straße 2 • 97828 Marktheidenfed • Germany
www.gabriele-publishing.com